## KUNUNUA KWA KADI YANGU YA eWIC

**Huenda usiweze kununua baadhi ya vyakula kwa kutumia WIC ikiwa:**

- ✓ chakula hicho si sehemu ya mafao ya WIC ya familia yako
- ✓ mafao yako yameisha
- ✓ bidhaa ya chakula haiko kwenye orodha iliyoidhinishwa na WIC

**Je, ninaweza kununua vitu visivyo vya WIC kwa wakati mmoja?**

Ndiyo. Tumia kadi yako ya eWIC kwanza. Kisha ulipie vitu hivyo vingine kwa njia nyingine. Tumia SNAP, kadi ya zawadi, pesa taslimu au kadi ya benki.

**Je, itakuwaje iwapo nadhani chakula cha WIC hakipo kwenye orodha iliyoidhinishwa na WIC?**

Ikiwa unaamini kuwa chakula ambacho kimeorodheshwa katika Mwongozo wa Vyakula wa WIC kiliachwa kimakosa kwenye orodha iliyoidhinishwa na WIC:

- ✓ zungumza na duka hilo
- ✓ zungumza na wakala wako wa ndani wa WIC
- ✓ nenda kwa **https://nyswicvendors.com**

Uliza ikiwa chakula hicho kinapaswa kuongezwa kwenye orodha iliyoidhinishwa na WIC.

**Je, ninawezaje kupata duka lililoidhinishwa na WIC?**

- ✓ Tumia **WIC2Go**, programu ya simu ya mkononi
- ✓ Uliza wakala wako aliye karibu wa WIC
- ✓ Tembelea **www.health.ny.gov/wic**
- ✓ Tembelea **www.nyswicvendors.com**

**Je, itakuaje iwapo nitahitaji mtu mwingine wa kunifanyia manunuzi ya WIC?**

Wape watu unaowaamini TU kadi yako ya eWIC na PIN.

## KUTUNZA KADI YANGU YA eWIC

**Je, itakuwaje ikiwa kadi yangu ya eWIC itapotea, kuibiwa au kuharibika?**

Batilisha kadi yako kwa kupigia simu Huduma kwa Wateja wa WIC kwa **1-844-540-3013**. Weka miadi kwa wakala wa eneo lako ili kupata kadi mpya.

**Je, ninatunzaje kadi yangu ya eWIC?**

**FANYA:**

- ✓ Hifadhi kadi yako. Utaitumia kila mwezi.
- ✓ Weka kadi yako salama na safi
- ✓ Hakikisha sehemu ya nyuma yenye mstari mweusi haina mikwaruzo.

**USIFANYE HAYA:**

- ✓ Kutupa kadi yako ikiwa umetumia mafaoyote. Utatumia kadi hiyo hiyo kila mwezi
- ✓ Kuhifadhi kadi karibu na sumaku au vifaa vya umeme kama simu za rununu
- ✓ Kuacha kadi kwenye jua au sehemu zingine zenye joto kama vile dashibodi ya gari lako

**Je, ni lini napaswa kupigia simu kwa Huduma kwa Wateja?**

- ✓ Ikiwa kadi yako ya eWIC itapotea au kuibiwa
- ✓ Ikiwa kadi yako ya eWIC haifanyi kazi
- ✓ Ikiwa mtu anatumia kadi yako ya eWIC bila ruhusa yako
- ✓ Iwapo unahitaji kujua mafao yako ya WICsalio au tarehe ya mwisho wa matumizi
- ✓ Ukisahau PIN yako
- ✓ Ikiwa ungependa kuweka upya PIN yako
- ✓ Ikiwa unahitaji usaidizi wa kadi yako ya eWIC

Taasisi hii inatoa fursa kwa kuzingatia usawa.

# MWONGOZO WA KADI YA eWIC JIMBO LA NEW YORK



NEW YORK STATE | WIC Program

## KADI YANGU YA eWIC NA PIN

### Kadi ya eWIC ni nini?
Unaweza kutumia kadi hii kununua vyakula vilivyoidhinishwa na WIC kwenye maduka ya WIC. Wakala wako wa ndani wa WIC ataweka mafao ya familia yako kwenye kadi yako.

### PIN ni nini?
PIN inawakilisha Nambari ya Kitambulisho cha Kibinafsi. Ni msimbo wa siri wa tarakimu 4 unaokuruhusu kutumia kadi yako ya WIC. Utachagua PIN yako unapowezesha kadi yako ya WIC.

### Je, ninapataje PIN yangu?
Ili kuwezesha kadi yako mpya ya eWIC na kuweka PIN, piga simu kwa Huduma kwa Wateja kwa **1-844-540-3013**. Utahitaji kujua:
- ✓ nambari ya kadi ya eWIC yenye tarakimu 16
- ✓ msimbo wako wa posta
- ✓ tarehe yako ya kuzaliwa

### Je, nitachagua vipi PIN yangu?
Chagua PIN yenye tarakimu 4 ambayo ni rahisi kwako kukumbuka, lakini ni vigumu kwa mtu kuikisia.

### Je, ninawezaje kuhifadhi PIN yangu kwa usalama?
- ✓ Hakikisha hakuna mtu anayetazama
- ✓ Usiandike PIN yako kwenye kadi yako ya eWIC
- ✓ Usiweke PIN kwenye pochi au mkoba wako

### Je! nikisahau PIN yangu au nikihitaji kuiweka upya?
Pigia simu Huduma kwa Wateja kwa **1-844-540-3013** au tembelea **www.EBTedge.com**. Utahitaji kujua tarehe yako ya kuzaliwa na msimbo wa eneo la posta.

### Je, itakuwaje nikiweka PIN isiyo sahihi kule dukani?
Una nafasi 3 zaidi za kuipatia. Ukikosea kwenye jaribio la 4, akaunti yako itafungwa. Hutaweza kutumia kadi yako hadi siku inayofuata. Au, unaweza kupigia simu Huduma kwa Wateja. Wataweka upya PIN yako.

## MAFAO YA KADI YANGU YA eWIC

### Je, ninapataje mafao ya WIC kwenye akaunti yangu ya WIC?
Katika miadi yako ya WIC, wafanyakazi wa WIC wataweka mafao yako kwenye akaunti yako ya WIC. Utapata orodha ya mafao ya WIC ya familia yako kwa muda wa miezi mitatu ijayo. Orodha hiyo itakuwa na tarehe za kuanza na kumalizika kwa mafao yako.

### Je, ni lazima ninunue mafao yangu yote ya WIC mara moja?
Hapana. Unaweza kununua vyakula vyako vya WIC jinsi unavyovihitaji.

### Je, kadi yangu ya eWIC inaweza kutumika tena?
Ndiyo. Weka kadi yako ya eWIC na uibebe kwenye miadi yako yote.

### Je, nitajuaje salio langu la mafao ya WIC na tarehe ya mwisho ya matumizi?
Kuna njia 5 za kupata taarifa hii:
- ✓ **WIC2Go**, programu ya simu
- ✓ risiti yako ya mwisho dukani
- ✓ tembelea dawati la huduma kwa wateja la duka lako
- ✓ pigia simu Huduma kwa Wateja kwa **1-844-540-3013**
- ✓ tembelea **www.EBTedge.com**

### Je, ikiwa nina swali kuhusu mafao zangu? Je, nikihitaji kubadilisha mafao yangu au fomyula ya mtoto wangu?
Waulize wafanyakazi wa wakala wa eneo wa WIC kuhusu kubadilisha mafao yako au fomyula ya mtoto.

### WIC2Go ni nini?
**WIC2Go**ni programu ya simu kwa Washiriki wa WIC wa Jimbo la New York. WIC2Go inaweza kukusaidia:
- ✓ Orodhesha miadi yako
- ✓ Angalia salio la mwezi wako wa sasa na tarehe ya mwisho wa matumizi
- ✓ Changanua bidhaa ili kuona kama vimeidhinishwa na WIC

**WIC2Go** inaweza kupakuliwa kutoka Apple App Store au Google Play.

## KUNUNUA KWA KUTUMIA KADI YANGU YA eWIC

Jinsi ya kutumia kadi yako ya eWIC unaponunua:

Hatua zinaweza kutofautiana kutoka duka hadi duka.

1. Chagua vyakula vya WIC kwa kutumia orodha yako ya ununuzi ya WIC, salio la mafao, Mwongozowa Vyakula na WIC2Go.
2. Chagua njia ya kulipa inayokubali WIC.
3. Weka bidhaa zako za WIC kwanza, mbele ya vyakula vingine.
4. Kagua risiti ya katikati ya malipo ili uidhinishe mafao ya WIC yaliyotumika.
5. Telezesha kadi yako ya eWIC na uweke PIN yako ya tarakimu 4. Usishiriki PIN yako na wafanyakazi wa dukani
6. Tumia njia nyingine ya malipo kwa bidhaa zisizo za WIC.
7. Hifadhi risiti ya dukani na kadi ya eWIC kwa ziara yako ya ununuzi ijayo.

